OFISI YA MWANASHERIA
MKUU WA SERIKALI

# OAG MAGAZETINI NA MITANDAONI WIKI HII

22/09/2025 ► 26/09/2025

OAG

WATANZANIA
ISSN 3057-3017 - TOLEO NA. 047 | ALHAMISI, SEPTEMBA 25, 2025 | THS: 1000
ELIMU BILA MIPAKA

# Rais TPBA aliamsha

- Atupa dongo kwa wanasheria wanaojimwambafai kuwa watafsiri wazuri wa sheria nchini
- Apigilia msumari kwa kusema hakuna mwanasheria anayewazidi wa serikali kwa kuwa wao ndio watengenezaji wa sheria, watafsiri

HABARI UK. 4



AG. Johari

Naibu AG. Masona




Rais wa TPBA, Bavoo Junus

# Rais TPBA aliamsha

NA JUMANNE SHABANI

RAIS wa Chama Cha Wanasheria wa Serikali Tanzania (TPBA), Bavoo Junus, aliamsha na kuwatupia dongo wanasheria wa kujitegemea wanaojimwambafai kuwa watafsiri wazuri wa sheria, wakati wanajua hakuna mwanasheria anayejua sheria kuliko wanasheria wa serikali.

Junus aliyaweka wazi hayo hivi karibuni, wakati alipokuwa akijibu swali na mmoja wa wahariri wa habari aliyetaka kujua ukimya wa wanasheria hao wa serikali kuhusu mambo mbalimbali yanayohusu serikali, pindi wanapotokea wanasheria wa kujitegemea kutaka kupotosha ama kwa makusudi au kwa kutojua tafsiri isiyosahihi.

Akijibu hilo, rais huyo alisema, "Suala la kubaka na kujibu kila hoja kwa maslahi mapana, tukaa na kujadili kuona namna ya kulifanyia kazi...lakini pia nizungumzie ukimya wetu huko nyuma kuwa ulichangiwa kwa kiasi kikubwa na kufuata miiko ambayo inatuongoza katika kazi zetu.

Pia tumekuwa tukikaa kimya kwa sababu, kukaa kimya napo ni jibu, ila pia ni kuondoa hali ya taharuki... sisi wanasheria wa serikali tunapojitokeza na kuzungumza au kutolea ufafanuzi wa jambo lolote kila mtu atalitafsiri kuwa msimamo wa serikali.

Tofauti ya hawa wanasheria wa kujitegemea iwapo atazungumza jambo la hovyo anaweza kubuka na kuomba radhi tofauti na sisi wa serikali ambapo ukikosea unakuwa umesababisha taharuki kubwa ambayo haitamalizwa kirahisi kwa kuomba radhi kama wafanyavyo wale wa kujitegemea.

Hii ndiyo sababu ya kuchelewa kujibu upotoshaji unaofanywa mara kadhaa na wanasheria 'warupokaji' ambao naamini mnawajua....

Kwani sisi huchagua jambo la kujibu hasa tunapoliona lina maslahi mapana ya taifa, baada ya kukaa na kujadiliana kwa kina na sio kuropoka kama wafanyavyo hao wa kujitegemea kwa kuwa hakuna anapofuatwa kama sisi wa serikali.

Napenda kuweka sawa kuwa hizi sheria zote sisi ndio waandaaji wake hivyo sidhani kama kuna mtu anaweza kuwa mtafsiri mzuri kutuzidi sisi, huyo mtu hayupo."

Hayo yanakuja katika kipindi ambacho kumekuwa na dhana potofu kutoka kwa Watanzania wengi wanaoamini kwamba wapo wanasheria wa kujitegemea hasa wanaojitokeza mara kadhaa na kuzungumza na vyombo vya habari wakikosoa baadhi ya mambo yanayohusu sheria kuwa wana uelewa mpana kuliko wanasheria wa serikali.

Wakati huo huo, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali imewataka Wahariri wa Vyombo vya Habari nchini kuzingatia maadili na kutumia kalamu zao kwa uadilifu katika kuhabarisha umma, kwa kuangazia umuhimu wa kulinda amani na usalama wa taifa wanapotekeleza majukumu yao ya kila siku.

Akizungumza hayo Mkurugenzi Msaidizi wa Uratibu, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Ipyana Mlilo, wakati wa kufunga kikao kazi kati ya Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali na Wahariri wa vyombo vya habari, kilichofanyika Septemba 12, 2025 jijini Dodoma.

Mlilo amesema kuwa Sekta ya Habari ni muhimu katika taifa, hivyo kupitia kikao hicho kimetoa fursa ya kuimarisha ushirikiano kati ya Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali na Wahariri, ili kufanikisha utoaji wa elimu kwa jamii kwa weledi.

"Kikao kazi hiki kimekuwa na manufaa makubwa katika kuhakikisha jamii inapata uelewa mpana kuhusu masuala ya kisheria. Tumejadiliana mambo mengi na yote yamepokelewa kwa uzito, tutayafanyia kazi kwa lengo la kuendelea kuelimisha umma." Amesema Mlilo.

> "Kikao kazi hiki kimekuwa na manufaa makubwa katika kuhakikisha jamii inapata uelewa mpana kuhusu masuala ya kisheria. Tumejadiliana mambo mengi na yote yamepokelewa kwa uzito; tutayafanyia kazi kwa lengo la kuendelea kuelimisha umma." Amesema Mlilo.

Akielezea majukumu ya Chama cha Mawakili wa Serikali Tanzania (TPBA) katika kikao kazi rais wa Chama hicho, Bavoo Junus Junus,

amesema kuwa TPBA ni nguzo muhimu katika kulinda, kusimamia na kutetea maslahi ya taifa na rasilimali zake.

Ameeleza kuwa TPBA ni chama cha kitaaluma kinachowaunganisha wanasheria wote wanaohudumu katika ofisi za umma ikiwemo halmashauri, wizara, wakala, taasisi za serikali na Kampuni ambazo Serikali ina hisa.

"Tuna jukumu la kuelimisha jamii kuhusu masuala ya sheria. Hili limefanikiwa kupitia Kampeni ya Msaada wa Kisheria ya Mama Samia, ambayo imetekelezwa kwa mafaniko makubwa katika mikoa yote ya Tanzania Bara na Zanzibar" amesema Junus.

Amefafanua kuwa TPBA, kupitia umoja wake, imeunda jukwaa la kuwaunganisha Mawakili wa serikali ambapo wamekuwa wakijadiliana kuhusu taaluma zao, pamoja na kutetea maslahi ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Aidha, amesema kuwa Chama hicho kimekuwa na utaratibu wa kutoa mafunzo endelevu kwa wanachama wake ili kukuza ufanisi na uelewa wa mfumo wa Sheria nchini, badala ya kusubiri waajiri kutekeleza jukumu hilo.

"Tumeendelea kutoa elimu ya Sheria kupitia vyombo mbalimbali vya habari na kuandaa makongamano ya kisheria yanayolenga kukuza uelewa wa jamii kuhusu masuala ya kisheria," amesema Junus.

Amesema kuwa TPBA kilianzishwa kwa mujibu wa Kifungu cha 16A(1) cha Sheria ya Utekelezaji wa Majukumu ya Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Sura ya 268, pamoja na Tangazo la Serikali Na. 889 la Agosti 16, 2019.

Aidha, Junus ameeleza kuwa TPBA na Chama cha Wanasheria Tanganyika (TLS) ni vyama viwili tofauti, ambapo TPBA ni chama cha kitaaluma kinachowaunganisha wanasheria wanaohudumu Serikalini pekee, ilhali TLS ni chama cha kitaaluma kinachowaunganisha wanasheria wote nchini bila kujali mwajiri wao.

Akizungumza kwa niaba ya Wahariri walioshiriki kikao kazi hicho, Mhariri Mkuu Clouds Media, Joyce Shebe, ameishukuru Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa kuratibu kikao kazi hicho ambacho kimekuwa na manufaa makubwa katika kuhakikisha wanakuwa na uelewa wa mambo mbalimbali ya kisheria jambo ambalo litasaidia kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi.



oagtanzania
www.oag.go.tz

SHERIA

# Sakata la TLS, polisi lachukua sura mpya

**Na Halfan Chusi**

CHAMA cha Mawakili wa Serikali (PBA) kimejibu kwa ukali hatua ya Chama cha Wanasheria Tanganyika (TLS) ya kuwataka mawakili wake kusitisha ushiriki katika kesi za msaada wa kisheria za jinai pamoja na shughuli zote zinazohusiana na mahakama na serikali.

Ni katika kile kinachoweza kufasiriwa kama mvutano wa kitaaluma wenye athari kubwa kwa haki za wananchi wa kipato cha chini.

Hatua hiyo ya TLS ilikuja kufuatia tukio la kushambuliwa kwa Wakili Deogratius Mahinyila ndani ya mahakama na askari waliodaiwa kumzuia asihudhurie kesi inayomkabili Mwenyekiti wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Tundu Lissu.

Kupitia taarifa yake kwa umma, TLS ilielekeza mawakili wake kutoshiriki katika huduma za msaada wa kisheria hadi hapo hatua za kisheria zitakapochukuliwa dhidi ya wahusika wa tukio hilo.

Lakini PBA, kupitia kwa Mwenyekiti wake, Ado November, imesema kwa msisitizo kuwa hatua hiyo ya TLS si tu kwamba ni kinyume cha sheria, bali pia ni ukiukwaji maadili ya taaluma ya uwakili, na ni ubaguzi dhidi ya wananchi maskini, na inatishia mfumo wa haki nchini.




Mwenyekiti wa Chama cha Mawakili wa Serikali, Wakili Ado Novemba, akizungumza na waandishi wa habari, jijini Dar es Salaam jana, kuhusu kupinga maazimio yaliyotolewa na Chama cha Mawakili Tanganyika (TLS). Kulia ni msaidizi wake, Stephen Charles. **PICHA: IMANI NATHANIEL**

**SHERIA YA MAWAKILI**

Akizungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam jana, Ado November alisema: "TLS ni chama cha kitaaluma. Uamuzi wake unapaswa kuongozwa na sheria, si hisia.

"Mawakili ni maofisa wa mahakama, si wanaharakati wa mitandaoni. Hatua waliyochukua si ya kisheria, si ya kikatiba, na si ya kiweledi."

Alisema kuwa kwa mujibu wa Kifungu cha 4 cha Sheria ya Mawakili (Sura ya 341 Marejeo ya mwaka 2019), kila wakili aliyeandikishwa ni mwanachama wa TLS kwa lazima, akiwamo Mwanasheria Mkuu wa Serikali na mawakili wote wa serikali.

"TLS si taasisi binafsi yenye mamlaka ya kukiuka sheria inavyoamua. Wajibu wake ni kulinda maslahi ya wanachama, kuhakikisha heshima ya taaluma na kusaidia upatikanaji wa haki - si kuzuia haki hiyo."

**MSAADA KISHERIA**

Mwenyekiti huyo alisisitiza kuwa huduma ya msaada wa kisheria si zawadi wala hisani ya TLS au wakili yeyote, bali ni matakwa ya sheria.

Alisema kuwa kwa mujibu wa Sheria ya Msaada wa Kisheria (Sura ya 21 Marejeo ya 2019), utoaji msaada wa kisheria ni jukumu la kisheria kwa taasisi zilizosajiliwa, ikiwamo TLS yenyewe.

"TLS imepewa dhamana ya uratibu wa msaada wa kisheria kupitia wanachama wake. Wanaposema wanasitisha huduma hiyo, wanawadhulumu moja kwa moja wananchi wa kipato cha chini na makundi maalum wasio na uwezo wa kulipia huduma hizo," alisema.

Aliongeza kuwa Kifungu cha 5(1) cha sheria hiyo kinalielekeza taifa kuhakikisha upatikanaji msaada wa kisheria kwa wote, huku Kifungu cha 6 na 7 kikiipa TLS jukumu maalum la kuratibu huduma hizo. Alisema uamuzi wa TLS ni wa hatari kwa mustakabali wa haki kwa wote.

**UKIUKAJI KATIBA**

Ado alidai hatua ya TLS inakiuka ibara kadhaa za Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, hususan: Ibara ya 13(1) inayosema watu wote ni sawa mbele ya sheria, na wanayo haki sawa ya kupata huduma za msingi bila ubaguzi.

Pia alirejea Ibara ya 26(1) inayomwelekeza kila raia na taasisi kutii Katiba na sheria zote za nchi.

"Kuwanyima msaada wa kisheria watu wa kipato cha chini ni ubaguzi wa wazi, unaokiuka Katiba. Ni uamuzi wa kiubinafsi usiozingatia haki, utu na usawa wa raia," alisema.

Alisisitiza kuwa TLS kama taasisi ya kisheria ina wajibu wa kufuata sheria na si kuongozwa na mihemko au matukio ya hisia.

Mwenyekiti huyo aliwatahadharisha baadhi ya viongozi wa TLS wanaotoa matamko ya kiharakati yanayopingana na taaluma ya sheria, akisema:

"Mawakili si wanaharakati wa mitandao. Kazi yao ni kulinda sheria na kusaidia jamii, si kutoa kauli za kuchochea mgawanyiko wa kijamii."

Alihoji mantiki ya TLS kuwaruhusu mawakili wanaopokea malipo kuendelea na kazi, huku wakipiga marufuku wanaotoa huduma kwa wahitaji. Kwa mujibu wake, hiyo ni ishara ya ubaguzi, ukosefu wa maadili na kuvuruga usawa wa kisheria.

**KIPIGO KWA WAKILI**

Akizungumzia tukio la kushambuliwa kwa Wakili Mahinyila, mwenyekiti huyo alieleza kuwa jambo hilo liko mikononi mwa vyombo vya dola na si jukumu la TLS kutoa hukumu au kuchukua hatua zinazoathiri haki ya wananchi.

"Tunaamini haki itatendeka kupitia mfumo wa sheria. Wakili ni ofisa wa mahakama. Anapaswa kuishi kwa mujibu wa sheria na si kutoa kauli za kugomea majukumu yake ya kisheria," alisema.

Alisisitiza kuwa taasisi yoyote, iwe ya mawakili au serikali, inapopaswa kuchukua hatua za kisheria, lazima izingatie Katiba, sheria za nchi na misingi ya haki kwa wote.

PBA imeonya kuwa vitendo vya taasisi kama TLS kuchukua hatua za kuwanyima wananchi huduma muhimu kwa sababu ya tukio linalohusu mtu mmoja ni hatari kwa utawala wa sheria, kwa kuwa vinawalenga watu wasiostahili kuadhibiwa.

"Wananchi wa vijijini, maskini, wajane, watoto - hawa ndio waathirika wa kwanza wa uamuzi kama huu. TLS inawanyima haki kwa visingizio vya kulinda heshima ya taaluma. Huu si uamuzi wa kitaaluma - ni uamuzi wenye ladha ya siasa," alidai.

**MSIMAMO PBA**

Kwa mujibu wa Ado, Chama cha Mawakili wa Serikali kitaendelea kutoa msaada wa kisheria kwa wananchi kama kawaida kwa sababu ni takwa la sheria, na si jambo la hiari.

Alisisitiza kuwa PBA ipo kwa ajili ya kuimarisha utawala wa sheria, kulinda maslahi ya Taifa, na kuwasaidia wananchi kupata haki zao bila ubaguzi.

"Tutatoa msaada wa kisheria bila kujali matamko ya kihisia. Tunafuata sheria, si hisia. Tumeanzishwa kwa mujibu wa sheria, na tutasimama na wananchi hadi mwisho," alisema.

Mvutano huu kati ya TLS na PBA unaibua mjadala mkubwa kuhusu nafasi ya taaluma ya uwakili katika kulinda haki, kuzingatia weledi na kudumisha misingi ya sheria na Katiba.

Wakati TLS ikisisitiza haki ya Wakili Mahinyila itendeke, PBA inakumbusha kuwa haki hiyo haiwezi kutetewa kwa kuvunja haki za wengine.

# Mawakili wa Serikali, TLS waingia kwenye mnyukano

Na Penina Malundo

CHAMA cha Mawakili wa Serikali (PBA) kimepinga vikali Chama cha Wanasheria Tanganyika (TLS) kwa utoa tamko lenye azimio la kutaka wanachama wake kusitisha kutotoa huduma za msaada wa kisheria kwa wananchi, kwani kwa kufanya hivyo ni kinyume cha sheria na ni kitendo cha ubaguzi na uvunjifu wa Katiba ya Nchi Ibara ya 13(1).

Kimesema kutoa msaada wa kisheria siyo suala la hiari, bali wakili anawajibu kwa mahakama na kwa watu wote wa ngazi zote wenye nazo na wasio nazo, hivyo TLS inawajibu wa kikatiba wa kutii Katiba na sheria kwa mujibu wa Ibara ya 26(1)ya Katiba.

Hayo yalisemwa jana jijini Dar es Salaam Mwenyekiti wa Chama hicho, Addo Mwasongwe wakati akizungumza na waandishi wa habari kuhusiana na maazimio yaliyotolewa na TLS kufuatia kushambuliwa mwanachama mweneza, Wakili Deogratius Mahinyila, akiwa kwenye viunga vya mahakama na watu wanaodaiwa ni Polisi.

Alisema hatua ya TLS ya kuacha kutoa huduma hizo kwa wananchi maskini si tu kwamba ni minyume cha sheria,bali pia inaleta hatari ya kuvuruga mfumo wa utoaji haki (Justice System)kwa wananchi walioko pembezoni.

Mwasongwe alisema nidhamu ya wakili ipo chini ya Kamati ya nidhamu ya mawakili kwa mujibu wa Advocate Act na si jukumu la baraza la TLS pekee.

"Kwa mujibu wa kifungu cha 13 cha Advocate Act (Cap.341) nidhamu ya mawakili ipo chini ya Kamati ya nidhamu ya mawakili (Advocates Disciplinary Committee) inayoundwa na Jaji wa Mahakama Kuu (Mwenyekiti),Mkurugenzi wa Mashtaka (DPP) na Mwanachama mmoja wa TLS.

'Hii inamaanisha kuwa nidhamu ya wakili si jukumu la TLS pekee bali ni jukumu la pamoja chini ya mahakama. Hivyo ni wajibu wa Kamati ya Nidhamu kuchunguza kauli au vitendo vinavyoweza kuashiria uvunjifu wa sheria au ukiukaji wa maadili ya kitaaluma,"alisema.

Alisema TLS ni chama cha kitaaluma chenye wajibu wa kuhakikisha weledi,ubora na heshima ya taaluma ya uwakili unadumishwa kwa mujibu wa TLS Act.

"Tunashauri kwa heshima ya viongozi wa TLS kuzingatia wajibu wao wa kisheria na kitaaluma na kuepuka maamuzi yanayoweza kuathiri haki za wananchi na heshima ya taaluma ya uwakili." alisema.

Mwasongwe alisema sheria Legal Aid Act(Cap.21 R.E 2019) inatamka wazi utoaji wa msaada wa kisheria ni jukumu la kisheria si tendo la hiari.

"Kwa mujinbu wa kifungu cha 5(1),Serikali na taasisi zilizosajiliwa zinzwajibu wa kuhakikisha upatikanaji wa msaada wa kisheria kwa wananchi.

'Kifungu cha 6 na 7 cha sheria hiyo kimeipa TLS jukumu mahsusi la kuratibu na kutoa msaada wa kisheria kupitia wanachama wake,"alisema

Aliongeza kuwa utoaji wa huduma za kisheria kwa wananchi zimekusudiwa kwa wananchi wa kipato cha chini na makundi maalum yasiyoweza kumudu gharama za uwakili.

Mwasongo alisema TLS kama taasisi ya kisheria inawajibu wa kikatiba wa kuhakikisha kwamba maamuzi yake hayapingani na sheria iliyoianzisha (TLS Act)na sheria nyingine husika kama Legal Aid Act.

"Katika ibara ya 26 (1) ya katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania 1977 inasema kila mtu anawajibu wa kutoo katiba na sheria za Jamhuri ya Muungano.

"Huku katika ibara ya 13(1)ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania 1977 inasema watu wote ni sawa mbele ya sheria na wanayo haki sawa bila ya ubaguzi wowote,hivyo kuwanyima wananchi wa kipato cha chini msaada wa kisheria kitendo cha ubaguzi (Discrimination) kinachopingana na Katiba ,kwa kuwa kinawanyima haki sawa ya kupata huduma za kisheria."alisisitiza

***Baadhi ya Wanachama TLS wafunguka

Wakili wa Kujitegemea, Diana Rwegasira alisema tamko lililotolewa na TLS sio zuri kwani TLS ni chama cha kisheria na taasisi ya kisheria na jicho la kisheria na ipo nchini Kisheria lakini cha kushangaza imetoa maamuzi ambapo hayapo kisheria.

Alisema suala la huduma za kisheria kusimamishwa si haki na si sawa kwa sababu ipo kinyume na sheria TLS ni taasisi mojawapo ya kisheria ambayo inajukumu ya kuhakikisha kwamba huduma hizo za kisheria inatolewa kwa wananchi.

"Jukumu la kutolewa huduma za kisheria sio la hiari ni matakwa ya kisheria ni kitu cha ajabu na cha kusikitisha na kuona kwamba wao TLS wapo kisheria na wanafanya kazi kisheria alafu wanakinzana na sheria.

"Hii sio haki ni unyanyasaji sio sawa kwani athari yake ni kwamba huduma za kisheria zinatolewa kwa wananchi hasa wale wenye kipato cha chini sasa unapositisha huduma kisheria unakuwa kama unawatenga ambapo ni kinyume na sheria na katiba kwa sababu Katiba ya nchi inasema kila mtu anahaki ya kisheri,"alisema

Rais Mstaafu TLS Wakili wa Kujitegemea,Francis Stolla, alisema maazimio kumi yaliyotolewa yalikuwa mazuri isipokuwa maazimio mawili hayaendani kisheria ikiwemo azimio la Wito wa Baraza la Viongozi kuwazuia wanachama wake mawakili na wanasheria wasijiusishe katika kutoa msaada wa sheria.

Alisema azimio hilo linahitilafu kwasababu linalenga wanachama wasitekeleze sheria Ibara ya 26 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Alitoa wito kwa TLS,ni vizuri kutetea haki za wanachama wake wanaoingia katika migogoro wakati wakifanya kazi zao za kutekeleza sheria,lakini Chama kisiwaingize wanachama wake katika mgogoro na sheria na kufanya wakiuke haki ya kuwasaidia wananchi.

# THBUB yataka wanahabari kujikita kuimarisha amani

Na Penina Malundo

TUME ya Haki za Binadamu na Utawala Bora Tanzania (THBUB) imetoa wito kwa vyombo vya habari kujikita katika kuimarisha amani,utulivu na demokrasia nchini kwa kutotumia vibaya kalamu zao.

Pia imewataka waandishi wa habari kuchukua tahadhari dhidi ya matumizi mabaya ya majukwaa ya habari ikiwemo mitandao ya kijamii.

Wito huo ulitolewa jana jijini Dar es Salaam na Katibu Mtendaji wa THBUB, Patience Ntiwa wakati akifungua mafunzo kwa Waandishi wa habari wa Mkoa wa Dar es Salaam kuelekea uchaguzi Mkuu Oktoba 2025.

Alisema waandishi wa habari wanawajibu wa kuepuka kutumia lugha ya matusi,kafsha,kejeli,udhalilishaji au vitisho katika kuripoti matukio ya uchaguzi.

Ntiwa alisema mbali na hayo waandishi wa habari wanapaswa kuepuka rushwa, takrima au zawadi zenye lengo la kushawishi maudhui yenye kuegemea upande wa chama au mgombea fulani.

"Mafunzo haya yatasaidia kuweka misingi ya kitaaluma na maadili kwa vyombo vya habari,waandsihi wa habari na wadau wote wa sekta ya habari kwa madhumuni ya kuhakikisha haki ,usawa na weledi katika utoaji wa taarifa kwa umma ili kukuza demokrasia nchini,"alisema na kuongeza

"Mafunzo haya yatasaidia kulinda amani na utulivu kwa taifa na kuepusha kuchapisha maudhui yenye viashiria vya uchochozi, upoteshaji, kuegemea upande mmoja au yasiyo na uthibitisho,"alisema.

Alisema katika kipindi cha uchaguzi,waandishi wa habari wanawajibu wa kuripoti habari na matukio yote ya uchaguzi kwa usahihi bila upendeleo kwa chama,mgombea au msimamo wowote wa kisiasa na kuweka uwiano sawia wa taarifa kwa vyama vyote vinavyoshiriki uchaguzi.

Ntiwa alisema katika muktadha wa uchaguzi ulio huru na wa haki na wenye kuzingatia misingi ya demokrasia,vyombo vya habari vinanafasi ya kipekee katika kuhakikisha kunakwepa upatikanaji wa taarifa sahihi kwa umma.

Alisisitiza kuwa vyombo vya habari ni daraja kati ya wagombea,vyombo vya siasa,Tume huru ya Taifa ya Uchaguzi (INEC) na wananchi ambapo vyombo hivyo vinachangia kwa kiasi kikubwa kujenga uelewa wa wapiga kura kuhusu sera na ajenda za kisiasa.

Kwa upande wake mmoja wa watoa mada katika mafunzo hayo,Kilua Mtae alisema haki za binadamu katika uchaguzi zimezingatia katika sheria mbalimbali za kimataifa,Kikanda na Kitaifa.

Alisema miongoni mwa haki hizo ni pamoja na kushiriki katika shughuli za umma,haki ya kutoa maoni,kutoa taarifa na kutobaguliwa.

"Katika mikataba ya kimataifa Tanzania ni miongoni mwa nchi ambayo imeridhia mikataba ya kimataifa ya kulinda haki za binadamu ikiwemo ibara ya 21 ibara ndogo ya kwanza inayosema haki ya kushiriki katika shughuli za umma,"alisema.

Naye Mtoa mada wa pili kutoka katika ofisi ya Tume hiyo, Philomeno Thomas alisema lengo la mafunzo hayo ni kuwakumbusha waandishi wa habari namna ya kutoa taarifa kipindi cha uchaguzi ikiwemo kufanya kazi kwa kuzingatia ukweli,kuripoti taarifa zilizosahihi na zilizodhibitishwa,uhuru na mgongano wa kimaslahi na kuhakikisha kuepuka kuandika kwa ushawishi na maslahi binasfi au kwa taasisi.

THE GUARDIAN
26/0/29025

# TFS lines up DPP, magistrates to handle forest cover offences

*"It is upon the prosecutors to make us see the big picture of the crime so that we are moved to deliver maximum sentences that are truly punitive"*

**By Correspondent Deodatus Mfugale, Morogoro**

LOCAL government authorities and the Tanzania Forest Services (TFS) agency have lately convened for a workshop on handling forest-related offences.

Tarsila Gervas, principal state attorney who opened the session and served as facilitator, said that forest conservation cannot succeed if forest officers work in isolation, addressing 32 officers from various institutions involved.

The officers were drawn from district forest departments, resident magistrate courts, and the Office of the Director of Public Prosecutions (DPP) for the training organized by the Lawyers Environmental Action Team (LEAT).

The training is part of an integrated approach for transformation of Tanzania's fuelwood value chain project, focused on strengthening investigation, prosecution and court procedures in forest crime cases, to close persistent gaps in law enforcement that undermine sustainable forest conservation, she explained.

"In this context, we should not expect forest officers to work alone and get results. They must team up with other institutions, including those in the judiciary, to ensure conservation efforts pay dividends so that communities are assured of livelihoods and the country realizes

TURN TO PAGE 2

FROM PAGE 1

economic and social development," she said.

Rampant deforestation is linked to illegal logging, with Tanzania suffering from the practice and serving as a transit route for timber harvested unlawfully in other countries, she stated, urging stakeholders to look beyond tree cutting and acknowledge the wider economic, environmental, and social impacts.

"Sustainable forest management has to strike a balance between conservation and development while empowering communities to protect their forests and benefit from them," she asserted.

Workshop participants expressed being vexed by the prevalence of light sentences or acquittals in cases related to forest cover offences, which the facilitator acknowledged, hinting that this is sometimes due to prosecution weaknesses.

"Evidence is the backbone of investigation—it must be authentic, complete, reliable and believable," she stated, asking prosecutors to prepare a case with a settled mind, without emotion or bias.

"If there is enough and strong evidence go ahead with prosecution; if there isn't, don't be in a hurry to prosecute," she explained, underlining a growing recognition that poor evidence collection and case presentation often enables offenders to slip through the cracks.

Dr Njilingi Makata, chief forest officer and a lecturer at Olmotonyi Forest Institute, pointed at a vivid disconnect between forest produce harvesting and enforcement of laws.

"Many charcoal producers do not understand the laws, rules and regulations governing forest conservation. At the same time, some institutions responsible for protecting forests, such as village governments and forest officers often fail to comply with the same rules in their daily work," she asserted.

Evod Soka, the Sengerema District senior resident magistrate acknowledged that courts often deliver light penalties in forest cases, and stressed that such sentences are guided by existing laws.

"It is upon the prosecutors to make us see the big picture of the crime so that we are moved to deliver maximum sentences that are truly punitive," he said. "Failure of which, our decisions are merely guided by what the law prescribes," he added.



oagtanzania
www.oag.go.tz

# Mawakili waonywa kutumia taaluma kama jukwaa la siasa

Na Tatu Mwakabana

CHAMA cha Mawakili wa Serikali (PBA) kimesema utoaji wa huduma za kisheria kwa umma si tendo la hiari, bali ni wajibu na jukumu la kila wakili nchini.

Kimesema hiyo ni kwa mujibu wa Kifungu cha 9 (1) cha Sheria ya Mawakili ambapo kila wakili aliyeandikishwa ni ofisa wa mahakama.

Mwenyekiti wa Chama cha Mawakili wa Serikali, Addo Mwasongwe alisema hayo jana alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari mkoani Dar es Salaam.

Mwasongwe alitoa kauli hiyo kutokana na kitendo cha Chama cha Wanasheria cha Tanganyika (TLS) kutoa tamko kuwa mawakili wote nchini wasitoe msaada wa kisheria kwa wananchi wenye uhitaji huo kutokana na tukio la wakili aliyekuwa akifuatilia kesi ya Mwenyekiti wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Tundu Lissu kupigwa na askari polisi nje ya eneo la Mahakama Kuu, Septemba 15, 2025.

Awali, TLS ilitoa tamko hilo la kutowasaidia wananchi wanaohitaji msaada wa kisheria isipokuwa kwa wale waliolipa fedha kwa mawakili ili kupata msaada huo.

Kwa mujibu wa Mwasongwe, TLS ni chama cha kitaaluma kilichoanzishwa kwa mujibu wa sheria na jukumu mojawapo kati ya majukumu yake matatu ni kusaidia upatikanaji wa msaada wa kisheria kwa wananchi.

Hivyo Mwasongwe alitaka TLS kufanya kazi kwa mujibu wa sheria na miongozo ya taaluma yao, kwa kufuata katiba ya nchi.

Aidha, aliongeza kuwa kwa kufuata miongozo hiyo ya kitaaluma, wakili hana mamlaka ya kutumia taaluma yake kama jukwaa la kisiasa au kwa vitendo visivyoheshimu sheria.

"TLS ni chama cha kitaaluma, ni vyema kila tamko na uamuzi wake uongozwe na weledi, ubora na utii wa sheria, badala ya msukumo wa kiharakati," alisema Mwasongwe.

Kadhalika, alisema kauli na maazimio ya TLS yanayolenga kuzuia mawakili wasitoe msaada wa kisheria ni kinyume cha wajibu wa msingi wa wakili kama ofisa wa mahakama na mtoa huduma kwa umma.

# CHRAGG calls for close cooperation with police to bolster human rights

By Polycarp Machira, Dodoma

THE Commission for Human Rights and Good Governance (CHRAGG) has reaffirmed its commitment to work with the Tanzania Police Force to strengthen protection of human rights and promote good governance across the country.

Speaking in Kondoa District, Dodoma Region yesterday, CHRAGG Chairperson Justice Mathew Mwaimu opened a training session for police officers and highlighted the importance of cooperation between the commission and law enforcement agencies.

He explained that the commission has consistently collaborated with police in delivering education on human rights principles and the rule of law.

"This cooperation is not limited to an organized training," he said. "It also includes our routine visits to police stations where we speak directly with detainees and ensure their rights are safeguarded."

Mwaimu emphasized that as Tanzania heads toward the 2025 General Election next month, the need for police officers to fully understand and respect human rights is critical.

"Our goal is to remind officers of their responsibility to protect human rights while carrying out their duties, particularly during this sensitive election period," he added.

He further explained that the training aims to refresh officers' knowledge of citizens' rights, professional conduct, and the constitutional obligations of the police force. According to him, public trust in law enforcement depends on adherence to these principles, especially when political activities increase during an election year.

Senior Superintendent of Police Desdery Rugimbana, Officer Commanding Kondoa District, praised CHRAGG for organizing the programme, noting that it will help officers perform their duties with discipline and fairness.

"This training will guide our officers in making sure they enforce the law while respecting the dignity of every individual," he said.

The session is part of a broader national campaign by CHRAGG to strengthen professionalism, accountability, and the rule of law in Tanzania. By equipping officers with updated knowledge on human rights and governance, the commission hopes to prevent abuses and promote peaceful and credible elections.

Mwaimu concluded by urging all participants to share what they learned with their colleagues in the field. He expressed confidence that such efforts will enhance relationship between police and the public, ensuring that citizens' rights are protected at all times and that the country maintains peace and stability during and after elections.

judiciarytanzania




**judiciarytanzania** JAJI MKUU AHIMIZA USHIRIKIANO KWA WADAU WA MAHAKAMA KUWEZESHA UTOAJI HAKI MAPEMA IPASAVYO

📌 Ni katika Mkutano wa Wadau kuhusu ushirikiano na Mahusiano katika Utekelezaji wa Majukumu ya Utoaji Haki mahakamani

📌 Asisitiza pia uwajibikaji wa wadau wa mnyonyoro wa haki

📌 Ashauri mikutano hiyo kufanyika angalau mara nne kwa mwaka

katibanasheria_



**katibanasheria_** UFUATILIAJI NA TATHMINI UIMARISHE UWAJIBIKAJI NA UWAZI

Katibu Mkuu Wizara ya Katiba na Sheria Eliakim Maswi amewataka watumishi wa Wizara hiyo kutumia ufuatiliaji na tathmini kama nyenzo ya kuimarisha ufuatiliaji, uwajibikaji na matumizi bora ya rasilimali.

Maswi ameyasema hayo Septemba 24, 2025 baada ya mafunzo ya umuhimu wa kufanya ufuatiliaji na tathmini yaliyofanyika katika ukumbi wa Wizara hiyo Mtumba jijini Dodoma ambapo ameongeza kuwa mafunzo yawezeshe watumishi kujipima utendaji wao.

tumesheria.tanzania



7

**tumesheria.tanzania** Tume ya Kurekebisha Sheria Tanzania imekutana na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali ya Zanzibar katika kikao kazi kilicholenga kuimarisha utekelezaji wa mkataba wa makubaliano ya ushirikiano (MoU) kati ya pande hizo mbili, kwa lengo la kuimarisha ushirikiano katika mapitio, maboresho, na utafiti wa sheria zinazotekelezwa katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar.

chraggtanzania




5

**chraggtanzania** HBUB KUENDELEA KUSHIRIKIANA NA JESHI LA POLISI

Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora itaendelea kushirikiana na Jeshi la Polisi katika kulinda haki za binadamu na utawala bora.

Kauli hiyo imetolewa Septemba 23, 2025 na Mwenyekiti wa Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora (THBUB) Mhe.Mathew Mwaimu wakati akifungua mafunzo kwa Maafisa wa Jeshi la Polisi Wilaya ya Kondoa, Mkoa wa Dodoma

oagtanzania




**oagtanzania** "Ushauri wa kisheria ulinde maslahi ya Umma — maarifa yatumike kwa vitendo!"

Mkurugenzi wa Uratibu na Huduma za Ushauri wa Kisheria Bi. Neema Ringo kwa niaba ya Naibu Mwanasheria Mkuu wa Serikali ametoa rai kwa Mawakili wa Serikali kutoka Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kutumia maarifa waliyopata kwa vitendo na kuhakikisha kuwa kila Ushauri wa Kisheria unaotolewa unalinda maslahi ya Umma na Taifa.

DAILY NEWS

# TPBA opposes TLS's restrictions on lawyers providing legal aid to the public

DOTTO LAMECK · 3 days ago 1,731




DAR ES SALAAM: The Public Bar Association (PBA) has strongly opposed a directive issued by the Tanganyika Law Society (TLS) which restricts lawyers from providing legal aid to the public.

The directive follows the September 15, 2025, assault of lawyer Deogratius Mahinyila by police officers while he was following up on a court cas involving CHADEMA Chairman, Tundu Lissu.


OFISI YA MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI TANZANIA
WELEDI NA UBORA
PROFESSIONALISM & EXCELLENCE
THE OFFICE OF THE ATTORNEY GENERAL TANZANIA
TUPO KARIBU YAKO!
Tufuatilie kupitia
oagtanzania
info@oag.go.tz
www.oag.go.tz
Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali
Mtaa wa Mtumishi
Mji wa Serikali Mtumba
S. L. P 630
Dodoma - Tanzania
KWA MSAADA WA HUDUMA ZA KISHERIA PIGA SIMU BURE 0800 11 0188
Weledi na Ubora